**Lukius Girabaya Mkobe, (1918 – 1989)**

Lukius Girabaya Mkobe alikuwa mwalimu na mchungaji nchini Tanzania. Alitafsiri vitabu kadhaa vya Ellen G. White katika lugha ya Kiswahili.

**Maisha ya Awali na Elimu**

Mnamo mwaka wa 1918, huko Nabihili, kijiji kinachopakana mikoa ya Arusha na Mara ya Tanzania, safari ndefu ya maisha ya mtu mashuhuri aliyeitwa katika Uadventista nchini Tanzania ilianza. Mara tu mtoto Lukius Mkobe alipozaliwa wazazi wake walihama kutoka Nabihili hadi kijiji cha Natta katika wilaya ya Mugumu, mkoani Mara, na nchini Tanzania. Waliishi huko kwa muda mfupi kabla ya wazazi wake wote wawili kufariki. Hili lilikuwa janga halisi na pigo kwa mtoto mchanga ambaye bado alikuwa katika hatua zake za mwanzo za ukuaji. Janga hili liliathiri ukuaji wake kimwili, kiakili, kiroho na kijamii. Hata hivyo, ukarimu wa Mungu haukumwacha mtoto huyu peke yake. Alikuwa amemuandaa mke wa mjomba aitwaye Sara Sasamwe kumlea yule mtoto mdogo aliyefiwa na wazazi.

Mnamo 1922, mama mlezi wa Lukius Mkobe alisikia Injili ya milele na akamkubali Yesu kama Bwana na Mwokozi wake binafsi. Mara tu alipoanza kuishi maisha mapya katika Kristo, shetani alimletea tufani hata akafukuzwa kutoka kwa familia yake kwa kukataa kujihusisha desturi za kikabila. Alipokuwa akienda zake, alikimbia na wasichana wake wawili na Lukius hadi misheni ya Waadventista Wasabato huko Ikizu, Ushashi, na Nyambitirwa zote mkoani Mara.

Mama yake wa kambo alimsajili katika Shule ya Msingi ya Ikizu mwaka wa 1929. Hii ilikuwa taasisi ya misheni ya Kanisa la Waadventista Wasabato. Baada ya kumaliza darasa la nane mwaka 1936, Lukius Mkobe alijiunga na kozi ya ualimu kuanzia mwaka 1937-1938 katika taasisi hiyo hiyo.

**Huduma ya Ualimu**

Ajira ya kwanza ya Lukius ilikuwa kuanzia 1939 – 1945 ambapo aliajiriwa kama mwalimu. Kanisa lilimpeleka sehemu ya kusini mwa Tanzania kuanzisha shule huko Mbeya. Kazi yake ngumu na ya ujasiri ya takriban miaka saba huko Mbeya wakati wa kipindi cha kutisha na kukatisha tamaa cha Vita vya Pili vya Dunia ilisababisha kuanzishwa kwa shule ya Waadventista huko Masoko, Tukuyu, Mbeya, Tanzania.

Mwaka 1946, Lukius alihamishiwa Kisiwa cha Ukara mkoani Mwanza, ambako alianzisha shule nyingine ya Waadventista. Hakukaa sana katika kisiwa hiki kwa maana alihamishiwa tena Malegea, Ukerewe, kisiwa kingine cha Mwanza kati ya 1947 na 1948, ambako alifanya kazi kama mwalimu mtaaluma akisaidia kupandisha hadhi ya shule na kufundisha waalimu. Hata hapa, Lukius hakukaa sana alihamishiwa tena Shule ya Msingi ya Bwasi iliyopo Majita, Musoma, Tanzania mwaka 1949 ambako alifanya kazi ya ualimu hadi mwaka 1953.

## Ndoa na Familia

Ilikuwa ni huko Bwasi Majita ambapo Mungu alikuwa amemuandalia Mchungaji Lukius Mkobe mwenzi wa maisha. Alimuoa Elizabeth Daudi Rubairo mwaka wa 1953. Mungu aliwabariki wanandoa hawa kwa kuwa na watoto kumi – mtoto mmoja wa kiume na wa kike tisa. Katika mwaka huo huo aliooa, alihamishiwa Ikizu kama Makamu Mkuu wa Shule. Alihudumu katika nafasi hii hadi 1957 alipoteuliwa kuwa mwalimu mkuu wa Shule ya Kati katika Shule ya Ualimu ya Ikizu. Lukius alikuwa na sifa ya kuwa Mwafrika na Mtanzania wa kwanza kujulikana kuwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Kati.

## Kazi ya Uchungaji

Lukius Mkobe aliendelea kuwa mwalimu mkuu hadi 1959, alipochagua kuitikia wito wa Mungu uliokuwa ndani yake wa kuhudumu kama mchungaji wa Injili. Hii ilimpelekea kuomba mafunzo ya uchungaji katika Chuo cha Bugema nchini Uganda. Chuo kilimkubali kwa sharti kwamba kwanza atumike kama mwinjilisti angalau kwa mwaka mmoja na kuripoti baadhi ya ubatizo unaotokana na kazi yake. Ili kutimiza sharti hili, alibadilisha kazi yake kutoka kwa mwalimu wa shule na, kwa wakati huu, mwalimu mkuu hadi uinjilisti na kumshuhudia Kristo. Kuanzia mwaka huu, kwa mujibu wa kitabu cha mwaka 1959 (Year Book), alianza kutambuliwa kama mchungaji mwenye leseni wa Misheni ya Tanganyika.

Uamuzi wake wa kufanya kazi kama mwinjilisti mlei ulimfanya ahamishe familia yake hadi Mwanza ambako alianza kushuhudia na kufungua kazi ya Uadventista Kirumba. Kazi yake nzuri iliwezesha kuanzishwa kwa kanisa la Kirumba na kusogeza huduma za kanisa karibu na baadhi ya watu ambao waliacha kuhudhuria ibada kutokana na kuelemewa na gharama ya nauli kutokana na safari ndefu ya kuja jijini Mwanza.

## Mafunzo ya Kichungaji na Utumishi

Kati ya 1960 na 1962, Lukius Mkobe alihudhuria mafunzo ya uchungaji katika Chuo cha Waadventista cha Bugema, ambacho sasa ni Chuo Kikuu nchini Uganda. Mara tu baada ya kuhitimu masomo yake, alipewa kazi kama mchungaji wa mstari wa mbele katika Kituo cha Misheni cha Utimbaru chenye makao yake makuu Kibumaye, na kama mwalimu mkuu wa Shule ya Kibumaye Middle School ambayo sasa inaitwa Muderspach Memorial huko Tarime, Mara, Tanzania, 1963. Mwaka uliofuata alihamishwa katika Kituo cha Misheni cha Shirati huko Tarime, ambako alihudumu kwa takriban miaka mitatu (1964 – 1966). Alihamishiwa tena katika Kituo cha Misheni cha Musoma, ambako alihudumu kuanzia 1967 – 1973. Vitabu vya Mwaka vya Waadventista (Year Book) kutoka 1965 hadi 1972 vinaonyesha kwamba Mchungaji Lukius Mkobe aliwahi kuwa Mjumbe wa Kamati ya Tendaji za Fildi za East Lake na Nyanza Mashariki. Alitawazwa katika huduma ya Injili kwa kuwekewa mikono ya kichungaji, mwaka 1966. Mchungaji Mkobe alianza kazi ya Waadventista pale Changamwe, Mombasa, Kenya, mwaka wa 1966, mwaka huo huo alipotawazwa.

**Masomo na Huduma Zaidi**

Mchungaji Mkobe aliendelea kujiendeleza kwa kujifunza zaidi masomo ya uandishi wa habari na uandishi wa vitabu kupitia mawasiliano kutoka Chuo cha Misheni cha Solusi, Bulawayo, Rhodesia Kusini, ambayo sasa inajulikana kama Zimbabwe. Programu hii ya masomo ilimchukua karibu miaka mitano kuanzia 1969 hadi 1973. Baada ya kumaliza masomo yake katika kiwango hiki, alipewa kazi ya kutafsiri miongozo ya kujifunza Biblia inayotolewa kila robo ya mwaka kutoka Kiingereza na kuipeleka kwenye Kiswahili na kisha kuituma Kendu Bay, Kenya, kwa uchapishaji. Baada ya kuchapishwa Mkobe alikuwa akienda kuichukua kutoka Kendu Bay na kuipeleka kwa viongozi wa Union Misheni ya Tanzania kwa ajili ya kuigawa. Pia alikuwa bora sana katika kutafsiri kwa Kiswahili mazungumzo ya wazungumzaji wa Kiingereza walipotembelea Union Misheni ya Tanzania.

Mchungaji Lukius Mkobe hakuridhika na kiwango cha stashahada ya uandishi wa habari. Kwa hiyo alisoma katika Chuo Kikuu cha Andrews kwa njia ya mtandao na kupata shahada ya Uandishi wa Vitabu kuanzia 1975 hadi 1978. Baada ya kuhitimu shahada yake, aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Uchapishaji na Sauti ya Unabii wa Union Misheni ya Tanzania kuanzia 1978 – 1984, akifanyia kazi zake kutokea Morogoro, Tanzania.

**Kustaafu**

Mchungaji Lukius Mkobe alistaafu kazi yake mwaka 1984. Alirejea kutoka Morogoro hadi Musoma ambako aliendelea na tafsiri ya vitabu mbalimbali vya Ellen G. White kwa Kiswahili. Maisha yake yaliisha mnamo Septemba 7, 1989, alipofariki akiwa na umri wa miaka 71.

**Urithi Aliotuachia**

Mchungaji Mkobe anakumbukwa kwa mambo mengi. Alitafsiri vitabu kadhaa vya Kiingereza kwa lugha ya Kiswahili. Vitabu alivyotafsiri ni pamoja na: *The Great Controversy*, kama Pambano Kuu; *The Desire of Ages*, kama Tumaini la Vizazi Vyote; *Counsels for the Church*, kama Nuru kwa Kanisa au Kutayarisha Njia Sehemu ya Kwanza; *Steps to Christ* kama Njia Salama; *Acts of the Apostles*, kama Kutoka Maonjo hadi Ushindi; na *Prophets and Kings* kama Mashujaa wa Imani au Wafalme na Manabii. Kitabu cha Nyimbo cha Kiswahili kiitwacho Nyimbo za Kristo kilitafsiriwa na Mchungaji Mkobe na Mchungaji Abihudi Mburuja.

Mchungaji Mkobe alitumika pia kama mjumbe wa Kamati ya Vijizuu vya Kiswahili akiwa pamoja na RC Megera, J. Kuyenga, na F. Martinsen.

Mchungaji Mkobe pia anakumbukwa kwa kuwafundisha watu muziki wa Kanisa. Wanamuziki wengi wazuri wa kanisa wa wakati wao kama vile Mchungaji Joktan Kuyenga, Fineas Majura Rubairo na wengine wengi ambao juhudi zao katika muziki

zilichangia maendeleo ya muziki wa kuabudu kanisani katika Kanisa la Waadventista Tanzania walipata mafunzo ya ustadi huu kutoka kwa Mchungaji Lukius Mkobe.